JINA ............................................................................ NAMBARI .....................................

DARASA ......................................................................... TAREHE .......................................

SAHIHI .......................................

102/3
KARATASI YA 3
OKTOBA 2019
MUDA: SAA 2½

# MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA KIDATO CHA TATU 2019

*(Hati ya Kuhitimu Kidato Cha Secondari.(K.C.S.E)*

102/3
KARATASI YA 3
OKTOBA 2019
MUDA: SAA 2½

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

**MAAGIZO**

(a) **Jibu maswali manne pekee**

(b) **Swali la kwanza ni la lazima**

(c) **Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi fupi.**

(d) **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

(e) **Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. **LAZIMA**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

MTU A: Tulienda kwa hiyo sherehe jana..

MTU B: Ooh! Kumbe ulipata ngiri mbili za kiingilio?

MTU A: Nilivaa chupa woiyee!

MTU B: Ulimwona yule kijana kamba?

MTU A: Hehehe! Yule huringa mbaya….

MTU B: Huyo alitoka mbio aliposikia kumethuka….

**MASWALI**

(a) Tambua kipera cha utanzu wa semi kinachohusishwa na kifungu hiki (alama 1)

(b) Eleza sifa <u>nne</u> za kipera ulichotambua katika (a) hapo juu. (alama 4)

(c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki (alama 5)

(d) Ngomezi ni nini? (alama 2)

(e) Eleza sababu ambazo zimesababisha kuzorota kwa matumizi ya ngomezi katika jamii ya kisasa (alama 5)

(f) Taja aina <u>tatu</u> za ngomezi ya kisasa (alama 3)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA B: RIWAYA

## CHOZI LA HERI (ASSUMPTA)

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Hili lilimtia ….. uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)

(b) Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili (alama 2)

(c) Eleza mbinu za lugha zilizotumiwa katika dondoo (alama 2)

(d) Kwa kutumia hoja <u>kumi na mbili,</u> eleza namna suala ulilolitaja hapo 2(b) juu linavyojitokeza katika riwaya (alama 12)

3. Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri.

(a) Kinaya (alama 10)

(b) Sadfa (alama 10)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA

## KIGOG: PAULINE KEA

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Mtalipa kila tone la damu mlilomwaga Sagamoyo; wewe na watu wako"

(a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

(b) Eleza sifa za mzungumzaji (alama 4)

(c) Thibitisha kwa kutoa mifano namna anayezungumziwa alivyomwaga damu (alama 12)

5. (a) Eleze mbinu ambazo jamii ya Sagamoyo ilitumia kupambana na uongozi mbaya wa Majoka (alama 10)

(b) Fafanua aina zozote **kumi** za migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya Kigogo (alama 10)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. **USHAIRI**

**Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali**

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Ni wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

**MASWALI**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (al. 1)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

(b) Fafanua dhamira ya mshairi (al. 1)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

(c) Kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote **mbili** za lugha zilizotumika Katika shairi (al. 2)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

(d) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi hili (al. 2)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

(e) Taja na ueleze bahari zozote **mbili** zinazojitokeza katika shairi hili (al. 2)

(f) Eleza toni ya shairi hili (al. 2)

(g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi (al. 4)

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

(h) Eleza umbo la shairi hili (al. 4)

(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi (al. 2)

(i) Malofa

(ii) Udubu

7. **USHAIRI**

Ni mimi nizamishaye chini
Mizizi kwenye majabali
Kufyonza chumvi!

Ni mimi ninyunyizae maji
Ili mimea ifumbue
Nafasi zao hewani
Ili miti ishike mamba kuzaa
Matunda, nafaka, mizizi na viazi
Ela mimi sili hata punje moja
Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,
Niliyeshiba madini
Ni mimi ninayechimba
Kupakua raslimani

Dhahabu, chuma, makaa..
ela yote yanaona
Yatiririka kwao!
Nabaki mtupu!

Vyakula vyote nazalisha mimi
Na mi' nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi
Na mi' nabaki u tupu!

Madini yote nawapa mimi
Na mi' nabaki kununua vyao!
Kazi zote nafanya mimi
Wao wabaki kunila nguzu!
Wao wanajita bora
Na mi' nabaki fukara!

*(Shairi la S.A. Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)*

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

7. (a) Lipatie shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(b) Fafanua aina **moja** ya taswira katika shairi hili (alama2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(c) Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(d) Huu ni ushairi wa aina gain? Toa sababu ya jibu lako (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(e) Eleza toni ya ushairi (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(f) Tambua tamathali ya usemi iliyotumiwa na mshairi kukuza Ujumbe kisha utoe mifano **miwili** (alama 3)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(g) Tambua nafsineni katika shairi hili (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

(h) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari. mishata katika shairi hili (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com

(i) Andika ubeti wa **pili** katika lugha ya nathari (alama 3)

**SEHEMU YA E: HADITHI FUPI**

8. "…. Hamna mwendawazimu wala mahoka kati yetu, mimi nimepewa zawadi hizo."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Eleza sifa nne za msemaji (alama 4)

(c) Hakiki nafasi ya maudhui ya busara kwa mujibu wa hadithi hii (alama 12)

for more free revision content visit: www.freekcsepastpapers.com